



Food and Agriculture  
Organization of the  
United Nations



# Mifugo yenye afya, Wafugaji wenye furaha!

Ugonjwa unapotokea, na dawa aina ya antibayotiki zikashindwa kufanya kazi, unaweza kupoteza Mifugo yako yote kutokana na ugonjwa.

Hii pia inahatarisha afya yako na familia yako kwani ugonjwa unaweza kusambaa kati ya Mifugo na binadamu.

## **Okoa maisha kwa kufuata ushauri uliopo hapa chini kuanzia leo!**

Kuna sababu kuu mbili zinazosababisha dawa zishindwe kutibu magonjwa;

- Kutumia dawa isiyo sahihi wakati wa matibabu husika au matumizi holela ya dawa.
- Vimelea vinavyosababisha maambukizi vinakuwa sugu dhidi ya dawa- kitendo hiki huitwa “Usugu wa Dawa”.

Kila tunapotumia dawa mfano Antibayotiki kutibu maambukizi kwa binadamu, mifugo na mimea, vimelea hawa hupata fursa ya kubuni mbinu mbalimbali za kukabiliana na tiba na kusabababisha dawa zipungue uwezo wa kutibu kadri muda unavyoenda.

Usugu wa dawa ni moja ya sababu kubwa inayosababisha dawa nyingi muhimu kushindwa kutibu ipasavyo. Tusipokuwa na dawa zinazofanya kazi vema, watu wengi, mifugo na mimea itakuwa katika hatari kubwa ya kufa kutokana na maambukizi.

**Lakini tunaweza kuchukua hatua sasa ili kuziwezesha dawa hizi kuendelea kufanya kazi ipasavyo!**

# Hatua kumi bora zinazofaa ili kuwa na mifugo na binadamu wenye afya na kuziwezesha dawa kuendelea kufanya kazi:



**1** Safisha banda muda wote kuondoa vimelea vinayosababisha maambukizi kwa mifugo na binadamu. Kumbuka **kusafisha mikono yako vyema, viatu na nguo** zako kabla na baada ya kushika au kuhudumia Mifugo.



**2** **Weka safi banda la Mifugo na mazingira yake kwa kuondoa** mboji na majani mara kwa mara. Uchafu wote unatoka kwenye mifugo iliyopewa dawa unahitaji kuondolewa kwa umakini.




**3** **Punguza hatari ya kusambaza vimelea.** Jitahidi kudhibiti watu kuingia bandani au kuwa karibu na mifugo yako na hakikisha unasafisha vifaa vilivyopo shambani. Tenga mifugo inayougua ili kuzuia maambukizi yasiendelee kusambaa.




**4** **Tumia mfumo wa kuingiza na kutoa mifugo kwa pamoja shambani** ili kupunguza hatari ya mifugo wapya kuambukiza mifugo iliyopo tayari shambani. zalisa na achisha mifugo yako kunyonya kwa wakati mmoja na endelea kufuga makundi haya ya mifugo kwa pamoja. safisha na tumia dawa ya kusafishia kabla ya kuingiza mifugo wapya bandani.




**5** **Tunza chakula cha mifugo mahali pakavu na salama** na weka mbali na wanyama waharibifu kwa mfano panya, ndege, wadudu na wanyama wengineo.



**6 Epuka visumbufu kwa mifugo.** Tunza vema mifugo yako na hakikisha wanakaa sehemu iliyo kavu yenye nafasi ya kutosha. Waache ndama wanyonye kwa muda mrefu kabla ya kuwaachisha ili kusaidia kuzuia maambukizi.



**7 Hakikisha mifugo yako inakuwa na afya njema** kwa kuwapa lishe bora ili kuzuia wasipatwe na maambukizi mara kwa mara. Tunza afya ya mifugo yako kwa kuwapa maji safi ya kunywa wakati wote.



**8 Toa chanjo kwa mifugo yako.** Pata ushauri kutoka kwa daktari wa mifugo namna bora ya kutoa chanjo muhimu na kwa muda sahihi. Kumbuka **“Kinga ni Bora Kuliko Tiba”**.



**9 Pata ushauri wa daktari wa mifugo kuhusu uchunguzi na matibabu sahihi ya Mifugo yako** kwa sababau kununua na kutumia dawa isiyo sahihi kunaweka afya yako, mifugo yako na familia yako katika hatari. Kutumia dawa isiyo sahihi ni kupoteza muda na fedha yako pia.



**10 Sambaza ujumbe huu na siyo vimelea!** Waambie wafugaji wengine ulichojifunza kwa sababu sote tunahitaji kufanya kazi kwa pamoja ili kuwa na ufugaji ulio bora, kulinda afya ya mifugo yetu, maisha yetu na afya za watu wengine wanaotegemea dawa zifanye kazi pale zinapohitajika kutumika.



**Unataka taarifa zaidi?**  
[www.fao.org/antimicrobial-resistance](http://www.fao.org/antimicrobial-resistance)  
twitter: @FAOAnimalHealth



Some rights reserved. This work is available under a [CC BY-NC-SA 3.0 IGO](https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/3.0/) licence